


# Maelezo Kuhusu Corona

Download hapa:  
[www.irenececile.com/covid19](http://www.irenececile.com/covid19)

## Je, virusi vya corona Covid-19 ni nini?

**Covid-19** ni virusi vipya vya aina ya corona. Mwili wa wagonjwa wa Covid-19 **unakolea moto na wanakohoa**. Kwa kawaida wagonjwa wa Covid-19 hawaumwi sana. Hata hauwezi kutofautisha na mafua au homa ya kawaida kama haujapima. Hata hivyo ni muhimu sana kujitenga na kukaa nyumbani ukiwa na dalili hizo. Ugonjwa huu ni rahisi sana kuambukizana. Halafu ugonjwa huu una hatari sana kwa watu ambao hawana afya njema. Hata vinaweza kusabibisha **kifo**.



Mpaka sasa **hakuna dawa** au chanjo. Hii ndio sababu watu dunia mzima wanajitahidi virusi hivyo visienee. **Je, na we unajiunga?**

## Je, watu gani wako kwenye hatari?

- Wazee
- Wagonjwa wa moyo
- Wagonjwa wa kifua
- Wagonjwa wa kisukari
- Wagonjwa wa figo
- Wagonjwa wa kansa
- Wagonjwa wa VVU/ UKIMWI




## Je, ninaweza kufanya nini kwa kusaidia?

Virusi vya Covid-19 vinaambukizana kupitia **mikono, kukohoa na kupiga chafya**. Unaweza kusaidia ili virusi visienee ukifuata sheria zifuatazo:



**Nawa mikono** na maji na sabuni kila mara.



Badala ya kutumia vitambaa ukiwa na mafua, tumia **tissue** na zitupe mara moja baada ya kuzitumia.


Kohoa au piga chafya kwenye **kifundo cha mkono**.



Usitoke nyumbani ukiwa **una homa, una mafua au koo inakuuma**.



Kaa mbali na watu wengine: angalau **foot 6**.



Hata ukijisikia poa, **penda kukaa nyumbani** na usipende kutembea ovyo.

Ikiwezekana epuka misongamano ya watu.



Kama **wote** tunafuata sheria hizo, virusi hivyo vipya vya corona **havitaenea haraka**. Lengo letu ndo virusi visiwafikii wazee na wagonjwa ambao wako kwenye hatari.